



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA
TAARIFA KWA UMMA**

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 20/04/2020.

Wizara ya Afya, Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya kumi na sita (16) wa Corona (COVID-19) nchini na kufikia idadi ya wagonjwa sabini na nne (74) kutoka hamsini na nane (58) ambao tuliowatolea taarifa tarehe 18 Aprili 2020.

Kati ya wagonjwa wapya, wagonjwa kumi na moja (11) wanatoka Unguja na watano (5) wanatoka Pemba. Kati ya wagonjwa hawa, wagonjwa kumi na tano (15) ni Raia wa Tanzania na mmoja (1) ni raia wa China.

Serikali kupitia wizara ya Afya, inaendelea kuwasilitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji ya kutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuakhirisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima. Tunawaagiza wananchi wote kuвая barakoa muda wote wanapotoka nje ya nyumba zao. Utaratibu wa uvaaji na barakoa na aina gani ya barakoa utatolewa na serikali.

Aidha Wizara inaomba wananchi ambao wana dalili za homa kali, kukohowa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya afya au kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo kutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyotokana na ugonjwa huu.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa huu wa COVID-19 kutoka Wizara ya Afya.

Ndugu wananchi tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kutuepusha na maradhi haya - Amin

Hamad Rashid Mohamed (MBM, MBLW)

Waziri wa Afya -Zanzibar